

# Kuzipa Kipaumbele Huduma za Matibabu Ili Kuendeleza Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi

## Kuhusu WeProsper

WeProsper ni muungano wa kimataifa unaoendeleza uwezeshaji wa wanawake kiuchumi (WEE, women's economic empowerment) kwa kushiriki katika shughuli za utetezi wa kimkakati ili kuendeleza usawa wa jinsia, kushughulikia vizuizi vya kimuundo na kupaza sauti na uwezo wa wanawake na wasichana kama wahusika kwenye uchumi. Kwa pamoja, tunajitahidi ili kujenga na kutumia mbinu za kimataifa zilizothibitishwa kuhusu uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kwa kutumia mbinu ya utetezi wa nadharia ya haki na usawa wa wanawake na jinsi utambulisho wa kijamii wa watu unavyoingiliana na kusababisha kuongezeka kwa hali za ubaguzi ili kumaanisha- kuchangia kikamilifu katika utunzi wa sera ya kimataifa, kuongeza ufadhili wa WEE, na kuendeleza ustawi wa wanawake na wasichana bila kujali tofauti zao zote.

Tafadhali changanua  
ili uone idadi ya wanachama  
wetu inayozidi kuongezeka



Kazi ya huduma ya matibabu imekuwa ikipendelea jinsia umoja kwa muda mrefu katika maeneo na tamaduni nyingi duniani, ambapo wanawake<sup>1</sup> na wasichana ndio wanaofanya kazi nyingi za nyumbani na za huduma ya matibabu bila malipo, ambacho ni kizuizi kikuu katika uwezeshwaji na haki zao kwa ujumla. Hii hasa ni hali inayotokea katika nchi zenye uchumi wa kiwango cha chini na cha wastani [LMIC, low- and middle-income countries], ambapo asilimia 75 ya kazi za huduma za matibabu za bila malipo na kazi za nyumbani hufanywa na wanawake, na ambapo wanawake huishia hutoa asilimia 90 ya huduma ya matibabu ya muda mrefu, ambayo kwa kawaida si ya kulipwa.<sup>2</sup> **Kuna ushahidi wa wazi: ikiwa huduma za matibabu bora na ya bei nafuu zitatolewa na mahitaji ya matibabu kushughulikiwa vizuri kupitia sera na ufadhili, hali ya uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, usawa na haki vitakuzwa.**<sup>3</sup> Kwa mfano, utoaji wa huduma ya matibabu ya hali ya juu kwa watoto unaweza kupunguza pengo la kimataifa la malipo ya jinsia kwa asilimia 8.6,<sup>4</sup> na uwekezaji wa asilimia 2.45 ya Kiwango cha Uchumi katika huduma ya matibabu ya muda mrefu unaweza kupunguza mapengo ya ajira ya jinsia kwa asilimia 7.4.<sup>5</sup>

Janga la COVID-19 lilionyesha na kuzidisha changamoto ambazo wanawake wanakabiliwa nazo duniani, hasa kuhusiana na kufanya kazi ya huduma ya matibabu bila malipo, na serikali na wafadhili walianza kutoa ahadi kuhusu huduma ya matibabu.

Hata hivyo, ahadi hizi hazijatekelezwa ipasavyo; uwekezaji lazima uzidishwe na kulengwa ipasavyo ili kushughulikia kikamilifu hali ya dharura ya kimataifa ya huduma ya matibabu na kuhakikisha hatua zinapigwa ili kuwezesha ufufuzi wa uchumi wa kudumu na wenye usawa. Kama sehemu ya hilo, uzingatiji wa vizuizi vya kimuundo vya kimsingi katika uwezeshaji wa wanawake kiuchumi ndani ya kazi ya huduma za matibabu ni muhimu. Suluhu zinapaswa kujenga mazingira bora kwa wanawake, kwa kuhakikisha kuwa kazi ya utoaji wa huduma za matibabu bila malipo inatambuliwa na serikali, kupunguzwa kupitia utoaji wa huduma bora na ya bei nafuu, na kusambazwa upya katika jamii, na kazi ya utoaji wa huduma za matibabu inayolipwa kuzawadiwa na kazi bora zaidi na kuwakilishwa kupitia miungano ya wafanyakazi.

Ili kusaidia katika utunzi wa sera, muhtasari huu unabainisha hoja muhimu kutoka kwa uchanganuzi wa utafuti wa hivi karibuni kuhusu huduma za matibabu uliofanywa na WeProsper kuhusu huduma ya matibabu ya watoto na huduma ya matibabu ya muda mrefu (LTC, long-term care), ambayo inajumuisha matibabu ya wazee na walemavu, na unatoa mapendekezo muhimu ya watunzi wa sera na wafadhili yanayolenga kuendeleza uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kimataifa (WEE, women's economic empowerment).

## R Tano (5) za Huduma ya Matibabu <sup>6,7</sup>

### *Kutambua, Kusambaza upya na Kupunguza*


kazi ya utoaji wa huduma ya matibabu bila malipo, kama vile:

- Kuzingatia kazi ya utoaji wa huduma ya matibabu bila malipo katika kufanya maamuzi, bajeti na ukusanyaji wa data
- Kusambaza kazi ya utoaji wa huduma ya matibabu kwa usawa kati ya wanawake na wanaume kuanzia nyumbani hadi kwa sekta ya umma
- Kupunguza kazi za utoaji wa huduma ya matibabu bila malipo ili kutoa muda zaidi kwa wanawake na wasichana kushiriki katika masuala ya siasa, uchumi na kijamii ambao kwa kawaida hubeba mzigo mkubwa zaidi wa utoaji wa huduma za matibabu

### *Kuzawadi na Kuwakilisha*

kazi ya utoaji wa huduma ya matibabu inayolipwa, kama vile:

- Kuhakikisha kazi bora na malipo sawa kwa kazi sawa
- Kuhimiza malipo, uwakilishi na uhuru wa kutosha wa kuunda miungano kwa wafanyakazi wa kutoa huduma ya matibabu inayolipwa



## Matokeo Muhimu kutoka kwenye Uchanganuzi wa Utafiti<sup>8</sup>

- Serikali zina jukumu kuu la kutoa huduma muhimu ya ubora wa juu, ya bei nafuu na inayoweza kufikiwa. Hata hivyo, uwekezaji katika huduma za matibabu haupevi kipaumbele katika nchi nyingi, na mara nyingi LMIC hukabiliwa na vikwazo vya nyenzo ambazo zinaweza kuwa muhimu kwa utoaji wa huduma hizo, hasa kutokana na athari za uchumi zilizosababishwa na janga la COVID-19.
- Wanawake hufanya kazi nyingi zaidi ya utoaji wa huduma za matibabu bila malipo, na usambazaji huu usio sawa wa kazi unaathiri uwezo wao wa kupata na kudumisha kazi, kusababisha kufanya kazi kwa muda mrefu, na unadunisha ustawi wao wa jumla.<sup>9,10</sup> Uwekezaji katika huduma bora ya matibabu ya bei nafuu kwa watoto na LTC unaweza kusaidia kupunguza na kusambaza upya kazi hii ya huduma ya matibabu, huku ukiendeleza uwezo wa wanawake wa kushiriki katika kazi ya kulipwa.
- **Uwekezaji katika huduma za matibabu hauendelevi tu usawa wa jinsia na kukuza ustawi; ni uamuzi wa sera ya kimkakati ya uchumi ambayo inasababisha ukuaji na nafasi nyingi za kazi, hasa kwa wanawake, na italipwa kwa sehemu na mapato ya ushuru.**

Uwekezaji katika huduma za matibabu unaweza kuunda nafasi nyingi za kazi na kusaidia kupunguza kwa kiwango kikubwa umaskini na utofauti wa malipo ya jinsi kuliko uwekezaji wa kawaida katika miundo mbinu, na kuendeleza ustawi wa pamoja na ukuaji wa uchumi.

- Kutoa huduma bora na ya bei ya matibabu ya watoto ni njia bora zaidi ya kuendeleza WEE, lakini kuna tofauti kubwa katika utoaji wa huduma hii duniani, hasa katika LMIC.<sup>11</sup> **Kimataifa, watoto milioni 350 wenye umri wa kuhudhuria shule ya msingi hawana uwezo wa kufikia huduma ya matibabu inayohitajika, asilimia 80 ya watoto hao wanapatikana katika LMIC.** Kuna kiwango kikubwa cha uwekezaji unaohitajika ili kujaza mapengo haya, kuanzia kwa asilimia 1.1 ya Kiwango cha Uchumi katika baadhi ya nchi, hasa katika nchi zenye uchumi wa kiwango cha juu hadi asilimia 14 ya Kiwango cha Uchumi katika nchi zingine. Kujaza mapengo haya kutasababisha manufaa mbalimbali kwa wanawake, kama vile kushiriki kwa kiwango kikubwa katika sekta ya ajira, nafasi mpya za kazi, kupungua kwa pengo la malipo, na kuongezeka kwa mapato ya familia.

- Kazi za LTC za bila malipo zinasababisha kikwazo kikubwa kwa WEE; ingawa, ikilinganishwa na huduma ya matibabu ya watoto, kuna uwekezaji mdogo katika LTC licha ya manufaa yake na kuwa asilimia 80 ya watu wenye ulemavu wanapatikana katika nchi za LMIC.<sup>12,13</sup> Katika baadhi ya nchi za LMIC, hakuna ufadhili wa serikali kwa huduma za LTC hata wakati ambapo idadi ya wazee inazidi kuongezeka.<sup>14</sup>
- Uwekezaji wa wafadhili katika huduma ya matibabu ya watoto na LTC umekuwa mdogo na mchache kufikia sasa. Kwa mfano, ufadhili unaolenga huduma na mipango ya matibabu ya watoto haupatikani kwa urahisi kupitia msaada wa maendeleo ya nchi na ufadhili kutoka kwa benki za maendeleo ya nchi, na mipango ya ufadhili kwa huduma za LTC ni michache hata zaidi. Mpango tofauti ni Mradi mpya wa Benki ya Dunia wa *Wekeza katika Matibabu ya Watoto (Invest in Childcare)*, ambao unaonyesha uwekezaji wa kiwango cha haja wa serikali katika matibabu ya watoto ambao utanza kujaza mapengo katika baadhi ya nchi.
- Sera zinazohusiana na matibabu za ulinzi wa jamii na sera za ajira na likizo ambazo zinazingatia jinsia, kama vile likizo inayolipwa ya uzazi, ni vipengele muhimu vya vifurushi vya sera ya huduma ya matibabu ambavyo vinaendeleza matokeo ya WEE. Kuna mapengo makubwa kimataifa kati ya huduma inayotolewa na nchi au mwajiri na bima kamili, ambayo inajumuisha huduma bora za jumla, bila malipo au za bei nafuu zinazozingatia jinsia.

### Ufafanuzi wa WeProsper wa Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi:

Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi (WEE, Women's economic empowerment) ni mchakato wa kuleta mabadiliko na matokeo ambao unaoruhusu wanawake kukuza uwezo wao halisi na kuthibitisha uwezo wao katika jamii na kuwa na usawa wa ufikiaji na udhibiti wa ujuzi, mali, nyenzo, nafasi, kufanya maamuzi na uwezo wa kujadiliana. Jambo muhimu kwa mchakato huu ni kuunda mazingira bora kwa kuhakikisha uwezo na uamuzi wa wanawake na wasichana na kushughulikia vigezo vya kimuundo vya uchumi ambavyo vinazuia usawa wa jinsia, ikijumuisha ajira na kusababisha usambazaji sawa wa kazi ya huduma ya matibabu ya bila malipo.

## Mapendekezo kwa Watunzi wa Sera na Wafadhili

**Zingatia zaidi uwekezaji katika matibabu ya watoto na huduma za LTC, ndani ya nyenzo zilizopo.** Serikali ni watoa huduma wenye jukumu la kuhakikisha usawa wa ufikiaji wa huduma ya matibabu. Kwa hivyo, watunzi wa sera wanapaswa kuzingatia zaidi na kupanua uwekezaji wa serikali katika matibabu ya watoto na huduma za LTC ili kuziba mapengo yaliyopo. Uwekezaji huu utasaidia nchi mbalimbali kufanikisha Lengo la Ukuaji Endelevu (SDG, Sustainable Development Goal) la Umoja wa Mataifa (UN) na kufanikisha lengo la bima ya jumla, kumaanisha huduma bora za matibabu kwa wote wanaozihitaji. Huduma hizo zinapaswa kuwa za bila malipo au za bei nafuu na kuhakikisha mahitaji ya wenye mapato ya chini zaidi na makundi ya wasiojiweza yanatimizwa. Suluhu zinazozingatia muktadha ni muhimu, na serikali zinapaswa kutumia utathmini wa mipango ambayo inaboresha matokeo ya WEE ili kubainisha mbinu bora ya kutunga sera.

**Kutoa ufadhili wa ziada wa serikali kwa huduma za matibabu kupitia uwekezaji wa wafadhili.** Kutoa msaada wa ziada kwa uwekezaji wa serikali, wafadhili, ikijumuisha taasisi za fedha za kimatifa na nchi zenye uchumi wa kiwango cha juu ambazo zinatoa msaada wa maendeleo, zinapaswa kuzingatia zaidi uwekezaji katika matibabu ya watoto na huduma za LTC ili kuendeleza WEE, pamoja na malengo pana ya maendeleo. Wafadhili wanapaswa kuunda mipango zaidi inayolenga matibabu ya watoto na huduma za LTC, kushirikiana na serikali na mashirika ya raia ili kuendeleza mipango iliyopo na kushughulikia mahitaji ya wasiojiweza zaidi. Ikifanikiwa, wafadhili wanaweza kuendeleza miradi kama vile *Wekeza katika Matibabu ya Watoto (Invest in Childcare)* ili kujaza mapengo ya huduma za matibabu.

**Lenga WEE katika utoaji wa huduma za LTC na matibabu ya watoto.** Katika kuizingatia jinsi ya kutunga sera za huduma za matibabu za kuleta mabadiliko, watunzi wa sera wanapaswa kukiri jinsi majukumu ya utoaji wa huduma za matibabu yanaathiri wanawake na wale wanaowahudumia kwa njia nyingi katika hatua mbalimbali maishani mwao, na kusababisha mapato ya chini ya kudumu na uwezo mdogo wa kifedha baada ya kustaafu kwa wanawake. Ili kupunguzia wanawake mzigo na kukuza huduma ya matibabu na ustawi wa watu wote kuanzia wakati wa kuzaliwa hadi kufa, serikali zinapaswa kuzingatia kutekeleza sera zinazokubali mbinu ya kudumu ya huduma za matibabu inayozingatia jinsi ambayo inaendelea malengo mapana ya utoaji wa huduma ya matibabu kwa wote na ulinzi wa jamii.

Pia, mipango inapaswa kujumuisha mahitaji mbalimbali na utathmini wa athari, kwa kulenga vigezo muhimu

vinavyoathiri uwezo wa wanawake na uhuru wa kutumia huduma za matibabu, ikijumuisha ufikiaji, ubora na nafuu.

**Kuunga Mikatiba ya ILO inayohimiza ulinzi wa watoa huduma za matibabu.** Serikali pia zinapaswa pia kutunga sera na kuunga Mikatiba ya ILO ambayo imethibitishwa kuendeleza matokeo ya uchumi ya usawa wa jinsia, kama vile likizo ya uzazi, familia na matibabu inayolipwa. Mifano inajumuisha Mikatiba wa ILO wa 190, unaolenga kuondoa vurugu na uchokozi katika mazingira ya kazi, na Mikatiba wa 189, unaotoa haki za msingi za kazi kwa wafanyakazi wa nyumbani.

**Utathmini wa mpango ili kubaini mapengo na kufuatilia maendeleo na athari zake kwa WEE.** Utathmini wa mapengo ya ufikiaji wa huduma ya matibabu, gharama na manufaa ya uchumi unapaswa kufanywa ili kutathmini mapengo wa huduma ya matibabu, ikiwa bado haujafanywa kwa kutumia zana zilizopo za sera kama vile, Mwongozo wa Wanawake wa Umoja wa Matifa wa *Guide to Public Investments in the Care Economy*.<sup>15</sup> Kuendelea kufanya utathmini ili kufuatilia na kupima maendeleo na kubainisha sehemu za kuboresha ni muhimu pia na unaweza kufanywa kwa kutumia zana kama vile Kadi ya Alama za Sera ya Matibabu (Care Policy Scorecard).<sup>16</sup> Serikali zinaweza kusaidia katika ukadiriaji wa maendeleo kwa kutoa data ambayo haijajumlishwa na kufanya utafiti wa matumizi ya wakati ili kubainisha athari ya kazi ya huduma ya matibabu kwa matokeo ya mpango wa Uwezesaji wa Wanawake Kiuchumi (WEE). Utafiti zaidi katika nchi na mipango mbalimbali, kwa kulenga nchi za LMIC, unahitaji pia kufanywa ili kufuatilia maendeleo na kuhakikisha uwekezaji bora na unaozingatia muktadha katika huduma ya matibabu ya watoto na LTC ambao unawezesha mpango wa WEE.

## Hitimisho

Dunia inaporejelea hali ya kawaida kutokana na janga la COVID-19, kukabiliana na changamoto mpya na mabadiliko ya idadi ya watu, na kujitahidi vile vile kuhakikisha usawa wa kiuchumi na haki za wanawake na wasichana, sera inayolenga huduma za matibabu ni muhimu. Serikali na wafadhili wana jukumu muhimu la kutekeleza na wanaweza kutumiwa mbinu nyingi zilizothibitishwa ili kutunga sera na mikakati ya uwekezaji ambayo inatambua, kupunguza na kusambaza upya ipasavyo kazi za utoaji wa huduma za matibabu za bila malipo na kuzawadi na kuwakilisha kazi za utoaji wa huduma ya matibabu za kulipwa.

## Marejeleo

- 1.**Moreira de Silva, J. (2019, March 18). Why you should care about unpaid care work. Development Matters, OECD. <https://oecd-development-matters.org/2019/03/18/why-you-should-care-about-unpaid-care-work/>
- 2.**Araujo de Carvalho, I., Beard, J., Chatterji, S., Jordan, J. E., Harvey, A., Keating, N., et al. (2015). World Report on Ageing and Health. World Health Organization. [http://apps.who.int/iris/bitstream/handle/10665/186463/9789240694811\\_eng.pdf](http://apps.who.int/iris/bitstream/handle/10665/186463/9789240694811_eng.pdf)
- 3.**Borrowman, M., E. Leasure, F. Papagiotti, K. Harris, and A. Nijhawan (2022). Global Assessment of Care Services: Current Status, Impact, and Policy Recommendations, WeProsper. Washington, D.C
- 4.**Eurasia Group. (2022, April 19). Reducing the global gender pay gap. Eurasia Group. <https://www.eurasia-group.net/live-post/we-could-reduce-the-global-gender-pay-gap-by-86-or-about-527-billion-if-high-quality-childcare-was-provided-to-all-women-around-the-world>
- 5.**De Henau, J. (2022). Costs and benefits of investing in transformative care policy packages: A macrosimulation study in 82 countries. ILO Working Paper 55. International Labour Organization. [https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---gender/documents/publication/wcms\\_839252.pdf](https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---gender/documents/publication/wcms_839252.pdf)
- 6.**Addati, L., Cattaneo, U., & Pozzan, E. (2022). Care at work: Investing in care leave and services for a more gender equal world of work. International Labour Organization. [https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---dcom-m/documents/publication/wcms\\_838653.pdf](https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---dcom-m/documents/publication/wcms_838653.pdf)
- 7.**Butt, A. P, Castro Bernardini, M. D. R., Parkes, A., Paz Arauco, V., Seghaier, R., & Sharmishtha, N. (2021). Care Policy Scorecard: A tool for assessing country progress towards an enabling policy environment on care. OXFAM. <https://oxfamilibrary.openrepository.com/bitstream/handle/10546/621287/bp-care-policy-scorecard-240921-en.pdf;jsessionid=ED3E9736C08C623A9FB69E51D5340736?sequence=17>
- 8.**Borrowman, M., E. Leasure, F. Papagiotti, K. Harris, and A. Nijhawan (2022). Global Assessment of Care Services: Current Status, Impact, and Policy Recommendations, WeProsper. Washington, D.C
- 9.**Moreira de Silva, J. (2019, March 18). Why you should care about unpaid care work. Development Matters, OECD. <https://oecd-development-matters.org/2019/03/18/why-you-should-care-about-unpaid-care-work/>
- 10.**Oxfam International. (n.d.) Not all gaps are created equal: The true value of care work. Oxfam International. <https://www.oxfam.org/en/not-all-gaps-are-created-equal-true-value-care-work>
- 11.**Devercelli, A. E., & Beaton-Day, F. (2020). Better jobs and brighter futures: Investing in childcare to build human capital. World Bank Group. <https://openknowledge.worldbank.org/bitstream/handle/10986/35062/Better-Jobs-and-Brighter-Futures-Investing-in-Childcare-to-Build-Human-Capital.pdf?sequence=5&isAllowed=y>
- 12.**OECD. (2019). Financing options to address women's unpaid care work. In Enabling women's economic empowerment: New approaches to unpaid care work in developing countries. OECD. <https://doi.org/10.1787/1dbd0046-en>.
- 13.**World Health Organization & World Bank Group. (2011). World Report on Disability. World Health Organization. <https://www.who.int/teams/noncommunicable-diseases/sensory-functions-disability-and-rehabilitation/world-report-on-disability>
- 14.**De Henau, J. (2022). Costs and benefits of investing in transformative care policy packages: A macrosimulation study in 82 countries. ILO Working Paper 55. International Labour Organization. [https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---gender/documents/publication/wcms\\_839252.pdf](https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---gender/documents/publication/wcms_839252.pdf)
- 15.**Ikkaracan, I. (2021). A guide to public investments in the care economy: Policy support tool for estimating care deficits, investment costs and economic returns. UN Women & International Labour Organization.
- 16.**Butt, A. P, Castro Bernardini, M. D. R., Parkes, A., Paz Arauco, V., Seghaier, R., & Sharmishtha, N. (2021). Care Policy Scorecard: A tool for assessing country progress towards an enabling policy environment on care. OXFAM. <https://oxfamilibrary.openrepository.com/bitstream/handle/10546/621287/bp-care-policy-scorecard-240921-en.pdf;jsessionid=ED3E9736C08C623A9FB69E51D5340736?sequence=17>



 [www.icrw.org/weproster/](http://www.icrw.org/weproster/)

 [@weprosterglobal](https://www.instagram.com/weprosterglobal)

 [@WeProsperGlobal](https://twitter.com/WeProsperGlobal)